


Mji mzima watu walikuwa wakiongea habari za uwezo wa Yesu.

Chini ya kila picha andika hadithi inayosimuliwa kwa kuangalia picha hiyo.



Miaka mingi kabla Yesu kuanza kazi yake, nabii Isaya alisema kwamba Masihi atakuja. Isaya

alisema hasa kile Yesu atakacho fanya. Soma Luka 4:18-19. Halafu kikate kifungu kisicho kweli.

Yesu atawahubiri maskini Injili.

Yesu atawapa vipofu kuona.

Yesu atawapa watu kuwa huru.

Yesu atajulikana na watu matajiri.


KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Alipokuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. Bali wote walio mpokea aliwapa uwezo wa kufanyi watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake." Yohana 1:11-12


Maneno hayo katika kifungu cha kukumbuka yenye mstari chini yao yanaeleza jinsi miji miwili mabalimbali ilivyompokea Yesu.

Ukiwa umemwamini Yesu na kumpokea, andika jina lako hapa: _____

Na ukiwa hujamwamini Yesu, uanweza kumwamini sasa hivi. Fanya kama watu wa Kapernaumu ambao walimpokea Yesu wakaufafhamu uwezo wake mkuu katika maisha yao. Waweza kuwa mwana wa Mungu leo kwa kumpokea Yesu moyoni mwako.



HATI YA KUVINGIRISHA



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved

Sura ya Kwanza

YESU ATEMBELEA MIJI MIWILI

MASOMO YA BIBLIA: Luka 4:16-44

"Yesu yuko nyumbani." "Yesu amerejea Nazareti." Habari hizi zilienea upesi kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine.


Watu wa Nazareti walikuwa wamesikia juu ya mafundisho ya Yesu na miujiza yake katika miji mingine. Sasa walitaka kusikia wao wenyewe kuwa mwana wa Yusufu atasema nini. Katika siku ya Sabato

Yesu alikwenda hekaluni kama ilivyokuwa desturi yake. Alisimama ili kusoma maandiko, akapewa kitabu cha nabii Isaya. Hakikuwa kitabu kama hiki tunachotumia siku hizi, bali ilikuwa hati ya kuingirisha ambayo alikunjua na kuisoma. Alisoma maneno haya juu ya mwokozi aliyeahidiwa:

"Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema.

"Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa!" Luka 4:18-19

Baada ya kusoma maneno haya, Yesu alikunja tena ile hati, akamrudishia kiongozi na kukaa chini. Ilikuwa desturi kwa msomaji hekaluni kusimama na kusoma neno



la Mungu, kisha kuketi chini na kueleza maana yake. Watu wote walimtamaza Yesu alipokuwa akijasoma maandiko haya.

Kati ya wale waliomsikiliza Yesu akisoma ni watu waliokuwa wamemfahamu karibu katika maisha yake yote. Watu wenye majivuno ambao hawakutaka kujifunza kwele mpya walikuwako pia. Walikuwa wamekwisha kusikia juu ya miujiza ya Yesu katika Kapernaumu, lakini hawakuamini ya kwamba alikuwa mwokozi hasa aliyeahidiwa. Yesu alikuwa ni mtu maskini na wao walimtamaza Mwokozi kuwa tajiri na mwenye uwezo.

Wote walikaa kinywa na kumgojia Yesu aseme. Walishangaa sana waliposikia maneno yake! Hawakujua kwamba aliweza kusema vizuri vile. Hawakujua kwamba alikuwa mwalimu mkuu wa ulimwengu.

Watu walipendeleza na maneno ya Yesu matamu na jinsi alivyozungumza, mpaka aliposoma, "Leo maneno ya Isaya yamekuwa kwele. Mimi ndimi nitakayehubiri Injili kwa maskini na waliosetwa, kuponya na kusaidia kama Isaya aliyoahidi."

"Hii inawezaje kuwa?" Walilulizana wao kwa wao. "Huyu siye mwanu wa Yusufu?" (Luka 4:22)

Yesu alijua kwamba hawangemwamini. Alisema, "Nabii habeshimiwi katika mji wake mwenyewe." Kisha aliwaambia habari za Eliya.

Alisema, "Siku mofa nabii Eliya alioroka kutoka Israeli kwenda kujificha katika nyumba ya mijane mmoja maskini katika nchi ya wapagani. Kwa sababu mijane huyu maskini alimtunza nabii wa Mungu, Mungu alimtunza yeye pia ingawa hakuwa Myahudi. Mungu alimponya Naaman, mpagani mwenye ukoma, alipoyatii maneno ya Elisha. Kulikuwa na wenye ukoma wengi katika Israeli wakati wa Elisha, lakini hakuna hata mmoja aliyeponywa ila Naamani.

Watu hawa wenye kiburi wa Nazareti waliposikia maneno hayo ya Yesu walikasisirikasana. Je, Yesu alikuwa akiwaambia kwamba Mungu aliwatunza watu wengine wasio Wayahudi. Walikataa kusikiliza maneno kama hayo! Walimruka Yesu kwa nia moja, wakamshika na kumtoa nje ya hekalu. Wakiwa wamejaa hasira walimchukua Yesu mpaka ukingo wa kilima ambacho mji wa Nazareti umejengwa juu yake, ili wantupe chini. Lakini Yesu alipita katikati yao akaenda zake.

Halafu Yesu alikwenda Kapernaumu, mji katika Gallilea, ambapo aliwafundisha watu katika sinagogi siku ya Sabato. Wote walishangaa mno jinsi alivyofundisha kwa kuwa maneno yake yalikuwa na uwezo.

Kulikuwa na mtu mmoja katika sinagogi aliyekuwa na roho ya pepo mchafu. Pepo yule mchafu alipaza sauti na kusema, "Tuna nini nawe Yesu wa Nazareti? Umekujia kutuunganiza? Nakujua wewe u

nani, Mtakatifu wa Mungu." Yesu alimwamuru yule pepo mchafu kumtoka yule mtu, na akamtoka. Watu wote walishangaa na habari zake zikaenea kila mahali katika nchi ile.

Yesu alitoka mle sinagogini akaenda nyumbani kwa Simoni.

Mkwewe Simoni alikuwa mgonjwa, na Yesu akamponya. Baadaya jua kuchwa, wote waliokuwa na marafiki wagonjwa waliwaleta kwa Yesu. Aliweka mikono yake juu ya kila mmoja akawaponya.

KAZI YA KUFANYA

(1) Taja mji ambamo Yesu alielewa.

(2) Tafuta jambo Yesu alilofanya katika mji huo. Kata kifungu kisicho cha kwele.

(a) Yesu alisimama kusoma maandiko hekaluni.

(b) Ilikuwa ni desturi yake Yesu kwenda hekaluni kila siku.

(c) Yesu alisoma kutoka kitabu cha nabii Isaya.

3. Yesu aliwaambia watu kuwa yeye ndiye aliyeandikwa habari zake na nabii huyo. Weka alama hii (X) kwenye mistari iliyo kando ya kifungu kinachoelewa jinsi watu walivyopokea habari hizo.

a. Waliliza, "Huyu siye mwanu wa Yusufu?" (Walikuwa na maana kwamba waliwajua wazazi

wake na kwamba hakuwa tofauti na wao.)

b. Waliamini kwamba Yesu alikuwa akisema kwele.

4. Mungu alimtuma Elisha kumponya mtu ambaye hakuwa Myahudi.

Piga mistari chini ya jina la mtu huyo.

Jona Naaman Isaka

Yesu aliondoka Nazareti akaenda Kapernaumu, Huko alikutana na mtu aliyeikuwa mwenye roho ya pepo mchafu. Andika alama hii (X) katika vifungu vya sentensi za kumaliza zilizo sawa.

Mtu yule aliyeikuwa mwenye pepo mchafu alikuwa

() mashuani

() sinagogini

() nyumbani

Yule pepo mchafu alisema kwamba Yesu alikuwa

() nabii

() Mtakatifu wa Mungu

Yesu alimkanya au alimkemea yule pepo mchafu, akasema,

() "Ulisema uongo"

() "Fumba kinywa, umtoke."

() "Omba!"

— Yesu alimwambia Simoni kusogeza mashua yao karibu na ukingo wa ziwa.

— Wanaume hao walikuwa wamevua usiku kucha bila kupata kitu.

— Simoni Petro alimtii Yesu kwa kushusha wavu kilindini.

Petro alikiri kwamatendo yake kwamba Yesu Kristo yu Bwana. Alijua kwamba Yesu alitaka nafasi ya kwanza katika maisha yake.

Unaaamini kwa moyo wako wote kwamba Yesu ni mwana wa Mungu aliyetumwa kutoka mbinguni kuwa Mwokozi wako?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Nakila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba." Wafilipi 2:11

Kifungu hiki kina maana kwamba siku moja kila mmoja atakubaliana na Mungu kwamba Yesu ni Mwanawe. Kisha watapiga magoti na kukiri kwamba Yesu ni Bwana.

Kama ndivyo, basi waweza kukiri sasa hivi siku ya leo kwamba Yesu Kristo yu Bwana. Hii ina maana ya kwamba unakubaliana na Mungu kwamba Kristo anastahili wewe kumwabudu na kumtii. Kubali kumpa Kristo nafasi ya kwanza moyoni mwako.

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

©Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved



Sura ya Pili

YESU AFANYA MIUJIZA ZIWANI


MASOMO YA BIBLIA: Luka 5:1-11

"Kuna nabii mgeni katika nchi yetu." Habari hizi zilienea upesi sana. "Afundisha juu ya Mungu na kuponya waponjwa pia!"

Siku moja Yesu alitembea kuelekea ziwa la Genesareti. Watu walikusanyika kumfuata. Pengine Yesu alikuwa amechoka. Pengine watu hao walifanya kelele nyingi na kusukumana walipokuwa waki-tembea. Lakini Yesu hakushindwa kuwavumilia. Alikuwa amekuja ulimwenguni kuonyesha upendo wa Baba yake kwa watu wote.

Hata ukingoni mwa ziwa watu waliendelea kusukumana ili wamkaribie Yesu. Walitaka wamwone kwa karibu. Yesu alianza kuwafundisha juu ya Baba yake wa mbinguni. Lakini watu wengine hawakuweza kumsikia.

Karibu na pale palikuwepo mashua mbili za kuvulia samaki. Palikuwepo na wavuvi wanne wakiosta nyavu zao; wavuvi hao wlaikuwa Petro, Andrea, Yakobo na Yohana. Yesu alingia katika mashua ya Petro. "Petro, waweza kuisogeza mashua yako mbali kidogo kutoka ukingoni?" Yesu aliuliza.




Petro alifurahi kufanya hivyo. Yeye na Andrea walisukuma mashua hiyo baharini.

Sasa watu wote waliweza kumwona na kumsikia Yesu. Walisikiliza kwa hamu maneno ya ajabu aliyowafundisha.

Baada ya Yesu kumaliza kuwafundisha watu hao waliosimama ukingoni mwa ziwa, alimgeukia Petro, akamwambai, "Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mnye samaki." (Luka 5:4b.)

Petro alimjibu, "Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini, kwa neno lako nitazishusha nyavu." (Luka 5:5) Petro na Andrea waliposhusha nyavu zao, waliweza kushika samaki wengi sana wakastaajabu.



"Njoooni mtusaidie!" Petro aliwaita Yakobo na Yohana. Kwa haraka hawa marafiki zao walikaribia kando ya chombo chao. Wakashika nyavu hizo ambazo zilikuwa zikikatika.

Wakaanza kuzivuta. Mara, mashua zote mbili zilikuwa zimejaa samaki hata wakahofu watazama.

Ndipo Petro alipoona hayo, alitambua ya kwamba Yesu hakuwa mtu wa kawaida tu. Aliigopa. Alimpigia Yesu magoti, akasema, "Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana!" (Luka 5:8)

Lakini Yesu alimwambia Petro, "Usiogope. Tangu sasa utakuwa mnyuvi wa watu."

Walipeleka mashua yao ukingoni, wakaivuta nje kisha wakaiacha pale ikiwa imejaa samaki, wakamfuata Yesu. Watu wengine wataweza kuchuka samaki hao. Petro, Andrea, Yakobo na Yohana walikwenda na Yesu. Walimfuata wakawa wanafunzi wake.

Siku moja baadaye, mkutano mkubwa wa watu walimfuata Yesu na wanafunzi wake. Yesu alianza kuwaeleza maana hasa ya kumfuata. Aliwaambia, "Mtu ye yote akianza kumfuata, sharti anipende kuiko anayopenda jamaa yake na hata yeye mwenyewe." Hili ndilo jambo alilifanya Petro.

Yesu aliahidi kufanya mvujiza kwa Petro ili aweze kuwa mnyuvi wa watu (yaani, mvitaji roho za watu). Kadiri Petro aliyoyjifunza kumweka Kristo kwanza maishani mwake ndiyo Kristo naye aliyozidi kuwa wa kwanza katika mambo yake yote.

Siku moja, baada ya Yesu kupaa mbinguni, Petro aliroa mahubiri. Kwa ujasiri mwingi aliliambia kundi

kutwa la watu kwamba Yesu Kristo ndiye Bwana. Siku hiyo watu wapatao 3,000 walimwamini Yesu. (Mateo 2:41)

KAZI YA KUFANYA:

Wiki iliyopita ulisoma juu ya miji miwili ambayo Yesu aliteembelea. Kati ya hiyo miji miwili ni mmoja tu ambamo watu walifurahi kumsikiliza Yesu. Andika jina la mji huo hapa.

Kisha Yesu alikwenda kwenye ziwa kubwa. Biblia inatoa majina matatu ya ziwa hilo. (Yohana 6:1; Luka 5:1) Yaandike majina haya kwenye nafasi iliyoko hapa.

Watu wengi walitaka kujua zaidi juu ya Yesu. Siku moja Yesu alipokuwa kwenye ziwa, makundi ya watu walimfuata. Andika jibu sawa kwa mstari ya kila swali.

Watu gani walimzunguka Yesu?

Walitaka kusikia nini?

Wavuvi walikuwa wakifanya nini?

Yesu alifundisha akiwa wapi?

(Majibu: Wakiosha nyavu, Neno la Mungu, Katika chombo cha kuvulia samaki, Watu wengi.)

Jibu maswali yafuatayo:-

Kama ungekuwa Petro ungeamini Yesu? _____

Kwa nini? _____

Hebu, fikiri juu ya mashindano yaliyokuwa katika mawazo ya Petro! Imani yake na akili yake ilikuwa na vita vikali. Ni kipi kilishinda vita hivyo? _____ Yesu alikuwa akimfundisha Petro kwamba, "Mambo yasiyowezekana kwa mwanadamu yawezekana kwa Mungu."

Yakate maneno yasiyo sawa katika vifungu.

Samaki waliingia wavuni hata ukaanza (kutanuka) (kukatika).

Kwa hivyo wale watu waliwaita (Yakobo na Yohana) (Yesu) kuja kuwasiaida.

Baadaye Yesu alifundisha kundi lingine la watu. Piga mstari chini ya kifungu kinachoeleza maana ya mafundisho ya Yesu.

"Mwaweza kuwa wanafunzi wangu mkiishi maisha bora zaidi."

"Hamwezi kuwa wanafunzi wangu msipojitoa na yote mliyvo navyo kwangu."

Baada ya Yesu kuwahubiria watu neno la Mungu alimpa Simoni Petro amri ya ajabu. Andika "K" kwa kwele au "M" kwa makosa mbele ya vifungu hivi.

alimokuwa _____

Kwa nini hawakumchukua kupitia
mlangoni?

Ukiwa umekwisha kumwomba
Yesu kukuokoa, atakusaidia kufanya
mambo ambayo yanaonekana kuwa
hayawezekani. Kwa mfano,
ukimpenda na kumtii, atakusaidia
kushinda hasira. Aweza kukufanyia
mambo usiyoweza kufanya wewe
mwenyewe.

Andika kwenye mistari ifuatayo
mambo utakayomkabidhi Yesu
akutendee wiki hii.

Je, ni jinsi gani walivyomfikisha
mgonjwa yule kwa Yesu.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Akasema, yasiyowezekana kwa
wanadamu yawezekana kwa Mungu."
Luka 18:27



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA

KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved

Sura ya Tatu

YESU NI TABIBU WA AJABU

MASOMO YA BIBLIA: Luka
5:12-26; 17:11-19

Kila mahali alipokwenda Yesu,
makutano makubwa ya watu
walimfuata. Siku moja palikuwepo
mtu mmoja maskini ambaye
hakuweza kuandamana na makutano
hao.

Alitaka sana kuponywa ukoma
wake! Hakuruhusiwa kuishi kati ya
marafiki na jamaa yake kwa sababu
angewaambukiza ukoma. Hakuruhu-
siwa hata kusogea kiasi cha kungusa
mtu ye yote asiye na ukoma kama
yeye. Lo! Haya yalikuwa maisha ya
huzuni sana.

Mtu huyu mwenye ukoma
alijuliza, "Sijui kama Yesu
ataniponya." Na kabla ya mtu ye yote
kumzuia, alimkimbilia Yesu akapiga
magoti kumsujudia. Alimsihi Yesu
akisema, "Ukipenda, Bwana, najua
unaweza kunitakasa."

Yesu alipomtazama mtu huyu
alitambua kwamba alikuwa
ameishisiku nyingi za huzuni mbali na
nyumbani kwake na ndugu zake
wapenzi. Yesu alijua vile mtu huyu
alivyokuwa katika hali ya upweke.

Yesu hakuogopa kungusa mtu
huyu kama vile watu wengine waliyoo
mwogopa. Kwa huruma alimwekea
mikono yake, akasema, "Nataka
kukuponya, takasika."

Mtu huyu aliinuka kwa haraka na
kusimama. Alikuwa na furaha na
shukrani tele kwa yale Yesu
aliyomtendea.

Katika amri ya Mungu ambayo
Musa aliwapa watu, Mungu aliamuru
kwamba watu wenye ukoma watoe
sadaka za shukrani wanapoponya.
Yesu alimwambia mtu huyu,
"Usimwambie mtu ye yote juu ya
haya. Nenda ukajionyeshe kwa
kuhani; ukatoe sadaka yakutakasika
kwako kama aliyoamuru Musa

kuhibitisha kwa kila mmoja kwamba umekwisha kutakasika."

Lakini habari za Yesu zilizidi kuenea. Makundi ya watu walikuja kumsikiliza akawaponya wagonjwa.

Na baadaye Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wakienda Yerusalemu walikutana na watu wengine kumi wenye ukoma. Watu hao walikuwa wamesikia kwamba Yesu anaponya wagonjwa. Hawakuweza kumsogelea Yesu kwa kuwa walikuwa na ukoma. Walipaza tu sauti zao kwa mbali wakisema, "Bwana Yesu, uturehemu."

Yesu hakupita tu bila kusimama. Aliwaambia, "Nendeni mkajionyeshe kwa makuhani." Walipokuwa njiani wakiwaendea makuhani wali takasika, miili yao ikapona.



Mmoja kati ya watu hao kumi wenye ukoma alisimama, akageuka kurudi alipoona kwamba amepona. Alianguka kifudufudi miguuni pake Yesu akamshukuru sana. Wale wengine tisa walifanya haraka kuendelea na safari yao bila kusimama kumshukuru Yesu. Yule aliyerudi kumshukuru hakuwa Myahudi bali Msamaria.

Yesu akasema, "walipoponya walikuwa watu kumi. Wale wengine tisa wako wapi? Kwa nini huyu mgeni pekee ndiye amerudi kutoka shukrani kwa Mungu?" Yesu alimwambia mtu huyu, "Inuka uende zako. Imani yako imekuoka."

Katika mji wa Kapernaumu kulikuwako mtu mmoja mgonjwa sana. Kwa sababu alikuwa na ugonjwa wa kupooza aliala kitandani wakati wote na hakuweza kuamka na kumwenda Yesu. Siku moja marafiki zake wanne walikuja, wakanwaza kitandani mwake, wakamchukua mpaka kwenye nyumba alimokuwamo Yesu. Lakini walipofika kwa nyumba hiyo hawakuweza kuingia ndani. Mkutano watu ulikuwa mkubwa mno.

Kwa hivyo walimchukua juu ya dari ya nyumba hiyo. Dari yenyewe ilikuwa tambarare na pia palikuwepo na ngazi ya kupandia juu yake. Walitoboa tundu katika dari hiyo, wakamshusha rafiki yao mgonjwa chumbani alimokuwamo Yesu.

Yesu alipoona imani waliyokuwa nayo, alimwambia mgonjwa huyo, "Mwanangu, dhambi zako zimesamehewa!"

Watu waliokuwepo walishangaa sana. Walifikiri ni Mungu peke yake ndiye awezaye kusamehe dhambi. Hawakuja kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu.

Kisha Yesu alimwambia mgonjwa huyo tena, "Inuka. Jitwike godoro lako uende nyumbani." Ndipo yule mtu aliposimama na kuitwaa godoro

lake na kwenda nyumbani. Alimtukua Mungu kwa kumponya.



KAZI YA KUFANYA

Kwa nini maisha ya yule mtu mwenye ukoma yalikuwa ya upweke mno?

Andika herufi "X" kwenye mstari ulio mbele ya jibu sawa la maswali yafuatayo.

Wale watu kumi wenye ukoma walikuwa wakiomba fedha.

Ndiyo. _____ La. _____

Wote kumi walimsihi Yesu awarehemie.

Ndiyo. _____ La. _____

Yote kumi waliponya ugonjwa wao wakarudi wote kumshukuru Yesu.

Ndiyo. _____ La. _____

Mtu mmoja tu aliyerudi (kutoka shukrani) alikuwa Myahudi.

Ndiyo. _____ La. _____

Piga mstari chini ya maneno ambayo Yesu alimwambia yule kiwete kwanza.

"Dhambi zako zimesamehewa."

"Simama uende."

Piga mstari chini ya sababu Yesu aliyoioa kwa kumponya yule kiwete.

Ili wale wanaotazama wajue kwamba Yesu ana uwezo kusamehe dhambi.

Ili kwamba yule kiwete awe mtumishi wa Yesu.

Piga mstari chini ya kifungu cha maneno kinachosema kile yule mtu alichofanya baada ya kuponywa na Yesu.

Alimwomba Yesu amponye mmojawapo wa rafiki zake aliyekuwa mgonjwa.

Alikitwaa kianda chake, akaenda zake nyumbani akimtukua Mungu.

Katika Luka 5:18 tafuta jinsi mgonjwa yule alivyochukuliwa na kupelekwa kwenye nyumba Yesu

mwanadamu. Waliuona utukufu wa ajabu alikuwa amepewa na Mungu.

Wanafunzi hawa watatu (Petro, Yakobo na Yohana walisikia pia sauti ya Mungu ikiwaambia kwamba Yesu ni Mwanawe mpendwa. Mungu alitaka wamsikie Mwanawe.

Pengine mnafikiria, "Ingalikuwa vema kama tungaliweza kumfahamu Yesu kama wanafunzi hawa wake walivyomfahamu!"

Waweza kuona utukufu mwingine wa Yesu katika Neno la Mungu. Waweza kumsikia Yesu akizungumza nawe leo. Unaweza kufanya hivi ukisoma Biblia yako. Waweza kumwomba Bwana kuzungumza nawe katika Shule ya Jumapili. Waweza pia kukariri vifungu katika Biblia ambavyo hukusaidia kufikiri habari za Yesu daima.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA

KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved

Sura ya Nne

YESU AFUNUA UTUKUFU WAKE

MASOMO YA BIBLIA: Luka 9:28-43

Yesu alifahamu kwamba baada ya muda mfupi atazifia dhambi za ulimwengu. Siku moja aliwachagua watatu kati ya wanafunzi wake kwenda naye kuomba. Petro, Yakobo, na Yonana ndio waliofuatana na Yesu mpaka juu mlimani.

Ilikuwa vigumu sana kupanda mpaka kilele cha mlima huo, na hatimaye walipowasili huko, walikuwa wamechoka sana. Mara tu walipofika kileleni Yesu alianza kuomba pamoja na wanafunzi wake kwa muda mfupi. Lakini wale wanafunzi walikuwa wamechoka sana kwamba kabla ya muda usio mrefu walikuwa wamelala. Halafu Yesu aliomba peke yake.

Yesu alipokuwa akiomba, kulitukia jambo la ajabu. Uso wake ulianza kung'aa kama jua, na mavazi yake yalikuwa meupe mno. Na kwa ghafula kulitokea watu wawili wakizungumza na Yesu, Musa na Eliya! Walikuja



kuzungumza na Yesu habari za kifo chake ambacho kilikaribia kutokea katika muda usio mrefu.

Watu hao wawili walipokuwa wakisema na Yesu wanafunzi wake walianka. Walsitaajabu kuuona utukufu wa Yesu wa kimbinguni. Haikuwachukua muda mrefu

kuwatambua hao wote ~~ngawa~~ kama walikuwa kina nani.

Musa na Eliya walianza kuondoka. Lakini Petro alitaka maajabu hayo yadumu zaidi. Kwa haraka alimwambia Yesu, "Bwana ni vizuri sisi kuwapo hapa. Acha tujenge vibanda vitatu hapa: kimoja chako, kimoja cha Musa, na kingine cha Eliya." Petro alipokuwa katika kusema, wingu lilishuka chini kutoka mbinguni likawafunika.

Wanafunzi walisikia sauti kutoka katika wingu. Waliogopa sana wakanguka kifudufudi. Mungu alisema nao, akawaambia, "Huyu ni Mwanangu, mteule wangu, msikieni yeye." Halafu kulinyamaa tena. Lakini wanafunzi waliendelea kuficha nyuso zao kwa sababu waliogopa.

Ndipo Yesu alikuja akawagusa wanafunzi wake. Aliwaambia, "Amkeni wala msioCOPE." Walipotazama, Musa na Eliya walikuwa wamekwisha kwenda na Yesu alikuwa peke yake. Yesu aliwakataza wasimwambie mtu yeye yote hayo waliyoana. Iliwapasa wanafunzi kuyaweka mambo haya siri moyoni mwao mpaka baada ya kufufuka kwake Yesu.

Sasa ulikuwa ni wakati wa Yesu na wanafunzi wake kukshuka mlimani. Walipofika chini ya mlima, kulikuwa na kundi kubwa la watu waliokuwa wakiwangoja. Mtu mmoja katika kundi hilo alikuwa akijitahidi sana amflic Yesu. Alipomkaribia, alipaza sauti, akasema, "Bwana, nakusihii unlazame mwanangu, kwa kuwa yeye ni mwanangu pekee. Nyakati

nyingine hupagawa na pepo mchafu naye hulia kwa sauti. Humia kifafa na kutokwa na povu kinywani mwake, wala hamwachi mpaka amemchubuchubua. Niliwasihii wanafunzi wako wamtoe huyo pepo mchafu lakini hawakuweza."



Mara tu baada ya Yesu kusikia habari hizo, alimwambia yule mtu amletee huyo kijana. Walipokuwa wakija, yule pepo mchafu alimshika yule kijana, akambwaga chini, akamitia kifafa.

Baba wa huyo kijana akasema, "Ukiweza, tukurumie utusidie." Yesu akasema, "Niliweza!" "Hiyo siyo shida. Swali ni kwanba, waweza kuamini? Yote yawezekana kwake aminiye."

Kwa upesi baba huyo alisema, "Naamini; nisaide kwa kutokuamini kwangu."

Yesu alimwamuru yule pepo mchafu amtoke yule kijana wala asimwingie tena. Ilimazimu yule pepo mchafu kumtaji Yesu, lakini alipokwisha kuondoka watu wote walidhani kijana amekufa. Yesu alimshika kijana kwa mkono akamwimua juu. Alikuwa mwenye

nguvu sana na yule pepo alikuwa amekwisha kumtoka.

Yesu na wanafunzi wake walipolingia nyumbani, wanafunzi walimwuliza kwa nini wao hawakuweza kumponya kijana huyo hali yeye aliweza. Yesu aliwambia, "Imani yenu ni haba. Iliwapasa kuomba na kufunga." Wanafunzi hao walikuwa wakijaribu kumfanya kazi Bwana Yesu bila kuwa na uwezo wake.

KAZI YA KUFANYA:

Siku moja Yesu aliwachukua wanafunzi wake watatu pamoja naye kuwaonyesha tukio ambalo hawangeweza kusahau. Kata neno lisilosawa katika vifungu vifuatayo na uandike neno lililo sawa katika nafasi zilizochwa.

_____ Yesu alipanda mlimani kulala.

_____ Yesu aliwachukua Petro, Andrea, na Yohana pamoja naye.

_____ Yesu alipokuwa mlimani sura yake ilibadilika na mavazi yake yakawa mekundu.

Andika herufi "X" mbele ya vifungu vilivyo sawa.

_____ Kijana alikuwa na pepo mchafu.

_____ Baba aliendelea kumpeleka mwanawe kwa madakari.

_____ Yule baba alikuwa amempeleka mwanawe kwa wanafunzi wa Yesu.

_____ Wanafunzi wa Yesu hawakuweza kumtoa yule pepo mchafu.

_____ Wanafunzi hawakujaribu kumsaidia yule kijana.

Wanafunzi wa Yesu hawakuweza kumsaidia yule kijana kwa sababu hawakuwa na imani ya kutosha.

Yesu alimwambia yule baba amfanyeje mtoto.

_____ Yesu alimfanya nini yule mtoto?

_____ Hii iliwafanya watu wote kuonaje?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Sauti ikatoka katika wingu, ikisema, 'Huyu ni mwanangu mteule wangu, msikieni yeye.'" Luka 9:35

Petro, Yakobo, Yohana, Musa na Eliya walimwona Yesu katika hali ambayo hajaonekana na mtu awaye yote. Mlimani walimwona Yesu kama Mungu na kadhalika kama

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA
MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA
KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved



Sura ya Tano

YESU AWATUMA WASAIDIZI SABINI

MASOMO YA BIBLIA: Luka 10:1-24

Tumekwisha kujifunza jinsi Yesu alivyowaita watu kumi na wawili kumsiadia kwa kazi yake wakati alipokuwa hapa ulimwenguni. Watu hawa waliitwa "wanafunzi." Pengine watu hawa walimfahamu Yesu zaidi kuliko mtu awaye yote. Walakini, Yesu aliwaita wengine pia kumsaidia. Siku moja Yesu aliwachagua wasaidizi sabini kumsaidia kwa kazi yake ya maana. Aliwapa maagizo au maongozi muhimu ya kufuata. Hebu tudhania kwamba tunamsikiliza Yesu na mmoja wa wasaidizi wale sabini wakizungumza juu ya kazi hiyo. Labda wanazungumza hivi:

Yesu: Nimewachagua ninyi kwa kazi maalum. Nataka mwende vijijini na kuwaambia watu kwamba naja.

Msaidizi: Lakini Bwana, kwa nini watutuma?

Yesu: Watu walio katika miji na vijijini ni kama mavuno mengi. Wako tayari kuletwa katika ufalme wa Mungu. Wakati huu ndio unaofaa sana kuwapelekea Injili watu hawa. Tukingojea tutachelewa.

Msaidizi: Lakini sisi tu watu sabini tu!

Yesu: Ndiyo, nafahamu. Ni lazima tuombe ili kwamba tuweze kuwa na watenda kazi wengi karibuni.

Msaidizi: Bwana, yatupasa kuchukua nini?

Yesu: Msichukue fedha zo zote wala vifaa vyenu. Msichukue viatu vingine. Chukueni tu vile mnavyovaa. Na mkikutana na watu njiani, msitumie wakati mwingi mkiamkuana nao.

Msaidizi: Lakini ni desturi zetu kuamkuana kwa kuinamisha vichwa vyetu na kuulizana hali ya kila jamaa.

Yesu: Mnayo kazi muhimu ya kufanya. Sitaki mtumie wakati wenu mwingi njiani mkiwatembelea jamaa.

Msaidizi: esu, tuseme nini tunapowasili katika miji na vijiji?

Yesu: Chagueni nyumba moja na mkae humo wakati mko katika kijiji kile. Mnapoingia nyumbani, semeni, "Amani iwemo nyumbani humu." Mle na mnywe cho chote watakachowapa.

Msaidizi: Ni kazi ipi tutakayofanya tunapowasili?

Yesu: Nataka mwaambie watu wajihuzunishie kwa ajili ya dhambi zao. Waambieni kwamba ufaime wa mbinguni umekariba. Pia nawapa uwezo wa kuwapaona wagonjwa. Mnapomponya mgonjwa semeni, "Tunakuponya kwa jina la Yesu" na mtu huyo atapona.

Msaidizi: Hii ni ajabu, Bwana. Watu wengi watatusikia na kukuamini. Lakini tuwafanye watu wanaokataa kuamini? Pengi hawatatukaribisha vijijini mwao.

Yesu: Mtu asipowakaribisha msijali. Myakung'ute mavumbi ya viatu vyetu na mtoke humo. Watajia ya kuwaba Bwana hakupendezwa. Ni lazima wajichagutie wenyewe. Lakini ni lazima mshiriki nao habari njema zisemazo kwamba Mwana wa Mungu yu hai.

Wasaidizi wale sabini waliondoka kwenda kufanya kazi walivyoambiwa na Yesu. Waliporudi walikuwa na furaha tele. Mmoja wao akasema, "Bwana, hata pepo wanatuii kwa jina lako." Walikuwa wamekwisha kushiriki Habari Njema na watu wengine. Walikuwa na furaha Kwamba Yesu alikuwa amewachagua kumsaidia.

KAZI YA KUFANYA:

Yesu aliwatuma wasaidizi wake kwenda vijijini kuantangulia. alisema ya kwamba watuambao wasaidizi wake waliwatembelea walikuwa kama mavuno yaliyo kondeni. Wakati huo ndio uliokuwa wakati wa Yesu kukudanya mavuno.

Chora duara kuzunguka matira ya ngano ambayo yako mbele ya sentensi iliyo kweli.



Yesu aliwatuma wasaidizi sabini kutembelea miji na vijiji.



Aliwatuma wasaidizi hao wake katika kundi la watu watata-watatu.



Yesu aliwaambia wasaidizi wake waombe ili kwamba watenda kazi wengine wengi waweze kutumwa.



Wasaidizi hawa sabini walishiriki habari Njema na watu vijijini na mijini.

Yesu aliwapa wasaidizi wake maagizo au maongozi muhimu. Andika namba ya maneno yaliyo hapo chini ili kukamilisha maagizo hayo ambayo Yesu aliwapa wasaidizi wake.

1. Misichukue
2. Mnapoingia nyumbani semeni
3. Mktanapo na watun njiani

msitumie wakati mwingi mkiamkuana.

fedha wala vifaa

"Amani iwemo nyumbani humu!"

Wasaidizi hao sabini waliporudi walikuwa na furaha tele. Katika picha iliyo hapo chini, mtu mmoja anamwambia Yesu mambo waliyoyaona katika safari yao. Jaza neno ambalo haliko kwenye nafasi iliyoachwa.

Bwana, hata pepo wanatuii kwa _____ lako.



KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Akawaambia, 'Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi katika mavuno yake.'" **Luka 10:2**

Yesu aliwachagua wasaidizi sabini kutembelea miji na vijiji. Aliwaambia wakahubirie watu habari zake. Siku hizi pia Yesu hutuambia tunde mambo yale yale.

Yesu ataka tushiriki Iojili na watu wengine ambao hawajui habari zake. Ametutuma kama vile alivyowatuma wasaidizi wale wake sabini. Ni lazima tuhubiri Habari Njema ya kwamba Yesu ndiye Mwana wa Mungu. Twaweza kuwasaidia watu kumjua na kumpenda Yesu. Sisi tu wasaidizi wa Yesu.




"Alimhurumia yule majeruhi."
Kifungu cha _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako." Luka 10:27

Yesu alisema kwamba jirani ni mtu ambaye ni mwema na ambaye huwaonea wengine huruma. Msamaria yule hakupendwa na Wahahudi. Lakini alisimama kumsaidia yule Myahudi aliyejeruhiwa. Alifanya hivyo kwa sababu alimpenda (huyo majeruhi) kama jirani yake.

Jirani zetu ni akina nani? Kila mtu ni jirani yetu. Na Mungu ataka tuwapende jirani zetu na kuwafanyia mambo mema. Twaonyesha upendo wetu kwa jirani zetu kwa kuwasaidia. Tukifanya hivyo tutakuwa kama yule Msamaria mwema aliyemsaidia Myahudi yule msafiri.



VJANA TUJIFUNZE BIBLIA MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

©Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved

Sura ya Sita

YESU AONYESHA NI NANI JIRANI MWEMA

MASOMO YA BIBLIA: Luka
10:25-37

Siku moja mwana-sheria mmoja mwenye akili alimwendea Yesu. Alikuwa akijaribu kumtega Yesu kwa kuuliza swali gumu zaidi. Alitaka Yesu atoe jibu lisilolingana na Agano la Kale, kisha Yesu ajiingize katika shida. Hapa pana swali hilo lake na sehemu ya jibu lake Yesu



Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?

Imeandikwa nini katika torati? Wasomaje?

Yesu alipomwuliza, "Imeandikwa nini katika torati?" Mwana-sheria

huyo alijua vema Agano la Kale, na akawa mwepesi kutoa jibu la haki. Alisema, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zaka zote; na jirani yako kama nafsi yako." Yesu akasema, "Umejibu vema. Fanya hivi nawe utaishi."

Mwana-sheria alijua kwamba hakutii amri hizo. Akauliza, "Na jirani yangu ni nani?" Yesu alijibu swali hilo lake kwa kumsimulia hadithi. Hadithi hii tunajua kwa jina la, "Msamaria Mwema."

Njia itokayo Yerusalemu kwenda Yeriko ilikuwa ya mteremko mkubwa. ilipitia pori ambayo ilikuwa na mapango na miamba mirefu. Njia hii haikuwa salama kupitia.

Siku moja fulani alikuwa akisafiri kupitia njia hii. Wanyang'anyi wengine walimwona wakakata shauri kumwimbia. Walimpiga na kumtia jeraha. Walichukua kila kitu

alichokwa nacho hata nguo zake. mtu huyu alichwa njia kama yu karibu kufa. Bila shaka mtu huyu aliomba mtu apite pale njiani aweze kumsaidia.

Mara palitokea kuhani mmoja aliyeshuka kwa njia ile. Kuhani huyu alipomwona hakusimama. Alipitia kando akaendelea tu na safari yake.

Kwa muda mchache, mtu yule aliyejeruhiwa alimsikia mtu mwingine akishuka kupitia njia ile. Mtu huyo alikuwa Mlawi, mtu aliyetumikia katika ibada ya kanisa. Labda mtu huyo angekuja na kumsaidia! Lakini Mlawi alipomwona alijiharakisha kwenda zake. Hakusimama ili amsaidie.

Yule mtu alianza kufikiri kwamba hakun mtu atakayemsaidia. Muda mchache baada ya yule Mlawi kupitia, msafiri mwingine akaja. Msafiri huyu alikuwa Msamaria. Nyakati hizo Wayahudi hawakupenda watu kutoka Samaria. Lakini jambo la ajabu lilifanyika. Yule Msamaria alimwona mtu huyu majeruhi, akasimama kumsaidia. Msamaria huyu mwenye huruma alimfunga jeraha zake, akamwimua juu. Alimpandisha juu ya punda wake, akampeleka mpaka kwa chumba cha wageni ili akamtunze.

Msamaria huyu alikuwa mwenye huruma mno hata akalipa fedha kwa mwenye chumba cha wageni ili yule majeruhi apate kutibiwa na kutunzwa. Wakati ulipofika wa Msamaria huyu kuondoka, alitaka hata kumlipia zaidi yule majeruhi ili apate utunzi mzuri. Alimpa mwenye chumba cha wageni fedha za

utumishi, kisha akasema, "Cho chote utakachogharimwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa."



Hadithi ilikomea hapo. Yesu alimwambia yule mwana-sheria, akamwuliza swali. "Wanaye wewe, katika hao watu, ni yupi jirani yake yule aliyeanguka kati ya wanyang'anyi?"

Pengine yule mwana-sheria pia hakuwapenda Wasamaria. Lakini alitoka jibu moja. Alisema, "Ni huyo aliyeuwonea huruma."

KAZI YA KUFANYA:

Agano la Kale lilitoa amri fulani kwa watu kufuata. Chora mistari kutoka sehemu ya kwanza ya amri hizo hadi kwa maneno yote yanayokamilisha amri hizo.

Mpende Bwana Mungu wako kwa

moyo fedha roho rafiki
nguvu akili

Mpende jirani yako kama wengine nafsi yako

Yesu alisimulia hadithi hii ili kuonyesha vile jirani mwema aliyo. Piga mistari chini ya maneno yaliyo kwei juu ya watu watatu waosimuliwa katika hadithi hii.

MTU FULANI

alishikwa na wanyang'anyi.
nguo zake zilibwa.

alijeruhiwa.

alikuwa karibu kufa.

KUHANI

alimwona mtu huyo aliyejeruhiwa.

alimpa huyo majeruhi nguo.

alipitia kando ya njia.

alimwomba majeruhi huyo.

MLAWI

alimtakazama majeruhi.

alipitia kando ya njia.

alimhurumia majeruhi.

alimpiga teke.

Piga mistari chini ya maneno ya kumalizia ambayo ni muhimu.

Jirani mwema

huwasaidia wengine ili nao wampende.

huwasaidia watu anaowapenda.

huwasaidia watu wenye mahitaji kwa sababu ampenda Yesu.

huwasaidia watu wenye mahitaji kwa sababu ataka ajisikie "vema".

Picha za hapo chini zaonyesha Msamaria Mwema akisaidia. Baada ya wewe kusoma vifungu vya Biblia, tazama picha hizo kwa uangalifu. Chini ya kila picha andika namba ya kifungu cha Biblia ambacho kinaeleza juu yake.



"Mtunze, nitakulipa." Kifungu cha



"Alifunga majeraha ya yule majeruhi." Kifungu cha

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA

KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

©Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved



Sura ya Saba

YESU AZUNGUMZA JUU YA HAZINA YA MBINGUNI

MASOMO YA BIBLIA: Luka 12:13-34

Kulikuwa na watu wengi ambao walikutana na Yesu wakati alipokuwa hapa ulimwenguni. Watu hawa wanaweza kutuambia mengi kuhusu mambo yaliyofanyika kati yao na Yesu. Dhania kwamba watatu kati ya watu hao walikutana na Yesu wanatuambia hadithi zao.

Wa Kwanza: "Nilikutana na Yesu siku moja alipokuja kijijini mwetu. Nilikuwa nimemkasirikia sana ndugu yangu. Baba yetu alikuwa amekufa akatuachia mali zake. Ndugu yangu hakunipa sehemu ambayo nilistahili kupewa. Nilimwendea Yesu kumwuliza kama



amekufa akatuachia mali zake. Ndugu yangu hakunipa sehemu ambayo nilistahili kupewa. Nilimwendea Yesu kumwuliza kama

angeweza kumfanya ndugu yangu kunipa sehemu yangu ya urithi. Yesu akasema kwamba hakuja kupatanisha watu katika ugomvi wao wa kindugu. Kisha akanifundisha somo zuri sana. Alinifundisha kwamba nistake mali nyingi kiasi ninachohitaji. Alisema, "Jilindeni na choyo." Yesu alinifundisha kwamba ni vibaya kutamani mali ya watu wengine. Nilikuwa katika tendo hilo la choyo."

Wa Pili: "Yesu aliponijia nilikuwa mkulima tajiri, Mwaka mmoja mavuno yalipatikana kwa wingi mno hata ghala zangu hazikutosha kuweka mavuno hayo. Nilikata shauri kuvunja ghala zangu ndogo na kujenga nyingine kubwa zaidi. Kisha ningeweza kuwa tajiri



kuwa tajiri

zaidi. Ningeweza kula, kunywa na kujiburudisha. Ningeweza kuwa na maisha mema. Lakini, kumbel! Nilikosea! Usiku ule nilipofanya mipango hii yote, Mungu alisema nami. Alinaimba, "Mpumbavu wewe, usiku huu wa leo utakufai! Na vitu ulivyojiweka tayari vitakuwa vya nani?" Nilifikirikaamba nilikuwa na kila kitu nilichotaka na kwamba ningeweza kuwa tajiri maishani mwangu mwote. Lakini kumbel! Nilikuwa maskini. Nilitambua kwamba tajiri ni yule anayemweka Kristo kwanza maishani mwake. Yule anayewafanya wengine mambo mema katika jina la Yesu. Nilikuwa mwenye choyo kwa hivyo sikuweza kufahamu mambo haya."

Wa Tatu: "Nilikuwa mmoja wa wanafunzi wa Yesu. Yesu alipomaliza kutusimulia hadithi ya mkulima mmoja tajiri hatukuelewa kwa sababu



s i s i
hatukuwa
tunatajirika.
Tulikuwa
tumeacha
kazi zetu ili
kumtumikia
Yesu.
L a k i n i
Yesu alijua
mioyo yetu.
A l i j u a

kwamba tulikuwa tunajaribiwa tuwe na wasiwasi. Alitambua, "Msisumbukie maisha yenu, mtakulal nini, wala mli yenu, mtavaa nini." Kisha akatambua habari za ndege wa angani. Ndege hawa hawapandi wala hawavuni. Mungu ndiye

anayewalisha. Nilitambua kwamba Mungu akiwa anawatunza ndege, basi atawatunza na watu pia. Yesu alitaka tumtegemee Mungu kutulinda. Si vizuri kuwa na wasiwasi. Yesu alisema kwamba kuwa na wasiwasi ni dhambi. Nilijifunza jambo muhimu sana siku hiyo!"

Watu hawa watatu wanaweza kutufundisha sisi sote mafunzo mema ya kufuata. Yesu alitaka tujue kuwa haitupasi kuwa na choyo. Pia alisema tusiwe na wasiwasi.

KAZI YA KUFANYA

Mtu mmoja alitaka sehemu ya urithi wake kwa tamaa zaidi kuliko vile alivyotaka upendo wake Mungu. Yesu alimwambia kwamba alikuwa akitenda dhambi. Piga mstari chini ya neno la dhambi ambalo Yesu alimwonya mtu huyu kwalo.

Kuwa Kudanganya Choyo Chuki

Mkulima yule tajiri pia alikukwa mtu mchoyo. Weka alama hii (X) katika nafasi zilizo kando ya sentensi zilizo kweli.

_____ Mavuno ya mkulima yule tajiri yalikuwa machache.

_____ Mkulima yule tajiri alikata shauri kujenga ghala kubwa zaidi.

_____ Alifikiri kwamba atakuwa maskini maishani mwake mwote.

_____ Mkulima yule tajiri alitaka kuishi maisha ya raha.

_____ Mungu aliondoa uhai wa mkulima yule tajiri kabla hajajenga ghala mpya.

Yesu alitumia mafunzo juu ya ndege ili kuwafundisha wanafunzi wake somo. Chora mstari kutoka kwa picha ya ndege huyo hadi kwa maneno aliyoyasema Yesu.



N d e g e
h a w a p a n d i
m b e g u w a l a
h a w a v u n i .
Mungu ndiye
anayewalisha
ndege.

Ikiwa Mungu anawalisha ndege hata sisi pia atatunza.

Yesu alisema kwamba kuwa na wasiwasi ni kubaya. Watu huwa na wasiwasi juu ya mambo mengi. Je, siku hizi watu huwa na wasiwasi juu ya mambo gani?

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa kuwa hazina yenu ilipo, ndipo itakapokuwapo na mioyo yenu." Luka 12:34

Wakati mwingine twatumia wakati wetu kwa kusudi la kupata vitu mbalimbali vya anasa mpaka tunakuwa wachoyo. Twataka tuwe na vitu au mali nyingi kuliko mahitaji yetu. Yesu alitambua kwamba inatupasa kuitafuta upendo wa Mungu kwanza. Tusitumie wakati wetu katika kujitafutia vitu vya anasa. Tutumie wakati wetu kuwatumikia wengine. Hili ndilo jambo ambalo Yesu alitaka tujifunze kutokana na watu hawa waliokuwa wachoyo.


VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA

KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

©Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved



Sura ya Nane

YESU AELEZA JUU YA KUTAFUTA KILICHOPQTEA

MASOMO YA BIBLIA: Luka 15:1-32

Kila mahali Yesu alipokwenda, makutano ya watu walimfuata. Mara nyingi Yesu alipowafundisha watu hawa aliwasimulia hadithi. Siku moja aliwasimulia hadithi tatu. Nazo zilikuwa juu ya vitu vilivyopotea. Hadithi hizo ni kama ifuatavyo:

Mchungaji mmoja alikuwa na kondoo mia moja. Siku moja aliwahesabu kondoo hao w a k e akapata ya kuwa mmoja alikuwa hayupo. Kwa h a r a k a alikwenda kumtafuta kondoo yule mmoja aliyeypotea. Alitazama na kutazama. Hata mwishowe akampata.



Alimbeba, akamweka mabegani mwake. Akamchukua nyumbani. Alipofika nyumbani alianza kufurahi. Aliwaambia jirani zake, "Furahini pamoja nami, kwa kuwa nimekwisha kumpata kondoo wangu aliyeypotea."

Kila wakati mwenye dhambi anapoacha dhambi zake na kumfuata Mungu, kunakuwa na furaha mbinguni. Mwenye dhambi ni kama kondoo aliyeypotea. Mungu ajaribu kumtafuta na kumrudisha nyumbani. Na mwenye dhambi anapookolewa kila mmoja mbinguni hufurahi.

Siku moja, mwanamke mwingine alikuwa na shilingi kumi. Alizitoa shilingi hizo kuzi-hesabu, naye akashangaa. Aligundua kwamba moja kati yashilingi hizo ilipote. Aliwasha taa



upesi na kuitafuta. Alitafuta kila mahali mpaka akipata. Na alipoipata alijiharakisha kwenda kwa jirani yake. Akamwambia, "Furahi pamoja nami, kwa kuwua nimeipata tena shilingi ile iliyonipotea."

Vivyo hivyo malaika wote mbinguni hufurahi wakati mwenye dhambi anapotubu dhambi, kama vile mwanamke yule aliyofurahi alipoipata tena shilingi yake.

Kulikuwa na kijana mmoja aliyejitayarisha kuondoka nyumbani kwao. Hakupenda maisha ya kishamba. Alimwambia baba yake, "Baba, nipe sehemu ya mali inayonianguka." Alaitaka kuchukua fedha zake na kwenda mjini. Alifunga wymba yake, akaondoka nyumbani. Alisafiri kwenda nchi ya mbali.

Haikuchukua siku nyingi kabla ya kijana huyu kutumia fedha zake zote. Alikaa huku katika maisha ya uasherati. Kisha jambo fulani baya lilitokea. Alipokuwa hana fedha, njaa kuu ilitokea. Ni watu tajiri tu ndio walokuwanachakula. Muda mchache kijana huyu alianza kusikia njaa. Alifikiri kutafuta kazi. Mwishowe akapata kazi ya kulisha nguruwe. Alikabiliwa zaidi na njaa hata akala chakula walichokula nguruwe.


Siku moja, alipokuwa akiwachunga nguruwe, alikata shauri kufanya jambo fulani. Angerudi nyumbani kwao! Alijua kwamba watumishi wa baba yake walikuwama maisha mema kumshinda. Alifikiria kurudi nyumbani na kumtumikia baba yake.

Safari ya kurudi kwao ilikuwa ndetu mmo kwake. Alikuwa mdhaifu kwa ajili ya njaa tena alichoka sana.

Alipokaribia nyumbani kwao, alimwonamtu fulani akija mbio kumlaki. Mtu huyu alikuwa babaye! Babaye huyu alimkumbatia. Alikuwa na furaha tele kumwona mwanawe. Lakini kijana alimwambia, "Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako. Sistahili kuitwa mwana wako tena."

Baba yake hakumruhusu aseme hivyo tena. Bila kutazamia yaliyopita alimwambia mtumwa wake akalete vazi lililo bora, viatu, napeteatiwe kidoleni. Aliwambia watumwa awake, "Mchijeni ndama yule tuliyewekea wageni waheshimiwa. Nasi tule na kufurahi kwa sababu mwanangu aliyekuwa amepotea ameonekana."

KAZI YA KUFANYA:



Mtu aliye pichani anatafuta kitu. Yeye ni mchungaji a m b a y e alipoteza kitu. Jibu m a s w a l i yafuatayo juu ya kile kitu huyu mchungaji alichopoteza.

Mchungaji huyu alikuwa na kondoo wangapi? _____

Wangapi waliopotea? _____

Alipompata kondoo huyu aliyepotea alimchukua nyumbani?

_____ Mchungaji huyu alifurahi pamoja na akina nani? _____ na _____

Yesu alisimulia hadithi ya mwanamke mmoja aliyepoteza kitu. Jaza nafasi zilizo katika hadithi iliyo chini juu ya mwanamke huyo.


Mwanamke mmoja alikuwa na shilingi _____. Lakini aligundua kwamba amepoteza _____ kati ya shilingi hizo. Kwa haraka aliwasha _____ na kuitafuta. Alipoipata, alikwenda kwa nyumba ya _____ yake. Akamwambia, _____ nami, kwa kuwa nimeipata shilingi iliyonipotea."

Piga mstari kutoka kwa picha ya mwana mpoovu hadi kwa kila sentensi ya kweli inayosimulia habari zake.

Alikaa, nyumbani na kufanya kazi shambani. Alitumia fedha zake kwa mambo ya uasherati. Alikuwa na chakula kingi cha kula. Alipata kazi ya kulisha nguruwe.

Alikula chakula alicho-walisha nguruwe. Alikata shauri kurudi nyumbani kwa babaye.

Hakusikitika kwamba alimtenda Mungu dhambi pamoja na baba yake.




KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuoka kile kilichopotea." Luka 19:10

Tupotezapo kitu fulani, yetu hututoka. Sisi huanza mara moja kukitafuta Ikwa bidii mpaka tunapokipata kitu hicho. Vitu vile tunavyopoteza ni vya muhimu kwetu. Na hivyo ndivyo alivyo Mungu. Hataki watu wapotee. Lakini ikiwa hatunjui Mungu na kumfuata tumepotea.

Yesu asema kwamba kila mmoja mbinguni hufurahi wakati mtu mmoja aliyepotea katika dhambi anapomrudia Mungu. Mungu hataki mtu ye yote apotee. Sisi sote tu muhimu kwake.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA
MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA
KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved

Sura ya Tisa

YESU ASIMULIA HADITHI JUU YA WATUMWA
WAAMINIFU

MASOMO YA BIBLIA: Luka
19:11-22


Yesu alifundisha kwa mafumbo mengi ili kuwasiaida wanafunzi wake wapate kuelewa vizuri mambo aliyokuwa akijaribu kuwafundisha. Siku moja, Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wakikaribia mji wa Yerusalemu, aliwasimulia hadithi juu ya mtu kabaila na watumwa wake watatu. Alisimulia hadithi hiyo kwa njia dhahiri mno hata wanafunzi wake wakaweza kuona mambo yaliyotokea.

Kabaila: Mimi ndimi kabaila niliyesafiri kwenda nchi ya mbali ili nipate ufalme. Kabla ya kuondoka, niliwaita watumwa wangu kumi nikampa kila mmoja fungu kumi la fedha kuniwekea mpaka nitakaporudi.

Baada ya kuwapa fedha hizo kuniwekea, niliondoka, nikaenda katika ufalme ule mpya. Hata hivyo, niliona kwamba singeweza kutawala ufalme ule mpya.

Watu walinichukia na hawakunitii. Walinitumia ujumbe wakisema: "Hatukutaki wewe ututawale."

Nilirudi katika nchi yangu, nikawaita watumwa wagu nijue faida waliyopata kwa fedha nilizowapa.



Mtumwa, umefanya nini fungu lako la fedha nililokupa?

Mtumwa wa Kwanza: Bwana, fungu langu la fedha ulionipa limelela faida kubwa, mafungukumi zaidi.

Kabaila: Vema sana. Wewe ni mtumwa mwema. Ulikuwa mwaminifu kaika kaika jambo hili dogo nililokupa. Nitakupa mamlaaka juu ya miji kumi, na hii itakuwa kama tuzo kwako.

Mtumwa wa Pili: Bwana, fungu langu la fedha ulionipa limelela faida kubwa - mafungu matano zaidi.

Kabaila: Vema. Wewe uwe liwali juu ya miji mitano. Je, na wewe mtumwa mwingine? Umefanya nini fungu la fedha nililokupa?

Mtumwa wa Tatu: Bwana, hilo ndilo fungu lako la fedha ulionipa. Nililiweka akiba kwa maana nilikuogopa kwa sababu ungetaka faida niliyopata. U mtu mgunu; waonda usichoweka, wavuna usichopanda.

Kabaila: Wewe ni mtumwa mwovu! Unasema mimi ni mtu mgunu? Basi, hivyo ndiyo nitakavyokutendea. Kama ulijua kwamba mimi ni mtu mgunu, niondoaye nisichoweka na kiyuna nisichopanda, mbona hukuweka fedha yangu kwa watoao riba, ili nijapo nipate pamoja na faida yake?

Watumwa, mnyang'anyeni huyu fungu hilo mkampe yule mwenye mafungu kumi zaidi ya fungu nililompa.

Watumwa Wale: Lakini, Byana, huyu ana fedha nyingi za kutosha.

Kabaila: Ndiyo, lakini nawaambia, kila aliye na kitu atapewa, bali yule asiye na kitu atanyang'anywa hata aicho nacho.


Yesu alisimulia hadithi hii kuwaonyesha wanafunzi wake ukweli. Mungu humpa kila mtu akili na uwezo kama vile kabaila aliyowafanya watumwa wake.

Sisi ni kama watumwa hao watatu wanaosimuliwa kaika hadithi hii. Baadhi yetu hutumia mambo yao yote kwa kuleta utukufu na faida kwa Mungu. Tunawahubiria watu habari za Yesu na kuwasaidia wengine wakati tunapoweza kwa sababu tunampenda Mungu. Tukitumia mambo yote kumtukua Mungu, Mungu atafurahi na kuhesabu kama watumwa waaminifu.

Wengine kati yetu ni kama mtumwa wa pili. Tunawahubiria watu habari za Yesu na kufanya matendo mema kaika jina lake, lakini hatufanyi hivyo mara kwa mara inavyotupasa.

Wengine hawashiriki habari za Yesu Kristona wenzao. Hatutumii akili na uwezo wetu kaika njia ya kumletea Mungu utukufu. Tuna ficha mambo yetu ili mtu mwingine ye yote asiweze kuvajua.

Yesu amempa kila mmoja wetu jambo la kufanya wakati huu ambapo tungali tunaishi hapa duniani. Anataka kuona kama tu waaminifu kaika jambo analotupa kabla ya kutupa jingine gumu zaidi ya hilo



Weka alama hii (X) katika mistari iliyo kando ya sentensi ambazo tunaweza kutumia kuonyesha tabia za mtumwa yule wa tatu.

_____ Hakufanya biasha fedha zilic alizopewa na bwana wake ili ampatie faida.

_____ Alifurahi kwa sababu alitenda haki.

_____ Aliadhibiwa kwa mambo aliyofanya.

_____ Alijaribu kumlaumu bwana wake kwa mambo yaliyofanyika.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA

"Nawaambia, Kila aliye na kitu atapewa, bali yule asiye na kitu atanyang'anywa hata aicho nacho." Luka 19:26

Inatupasa kutumia mambo yote ambayo Mungu ametupa kwa utukufu na heshima yake. Tukifanya hivyo, tutafurahi na kuona fahari wakati atakapotuuliza kueleza mambo kyote ambayo tumekwisha kufanya. Ikiwa bado hatujamtumikia Bwana kama inavyotupasa, labda tutaona aibu na pengine kufukuzwa kama mtumwa yule wa tatu.

KAZI YA KUFANYA:
Piga mistari chini ya majibu yaliyo sawa:
Kabaila alisafiri kwenda nchi ya mbali kutafuta mke.
Kabaila alimpa kila mtumwa wake almasi najohari kumweka wakati alipokuwa amcondoka.

Watumwa wake wawili walimpatia faida, akawatuza.

Mtumwa wa tatu aliweka fedha aliyopewa na bwana wake kwa watoao riba ili ajapo apate faida yake.

Kabaila aliwaadhibu watumwa wake wote watatukwa mambo waliyofanya.

VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA

KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

©Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved



Sura ya Kumi

YESU AFUNDISHA JUU YA MAOMBI

MASOMO YA BIBLIA: Mathayo 6:9-13; Luka 11:5-13


Mara kwa mara Yesu aliwafundisha watu juu ya maombi. Ilikuwa jambo la muhimu kwa wanafunzi wake kuelewa maana ya maombi na jinsi ya kuomba. Hata siku moja aliwapa mfano wa kuomba. Mfano huu twaita "Sala ya Bwana." Je, wajua sala hii kwa kichwa?

Hii ndiyo sala ambayo Yesu alitumia kuwafundisha watu jinsi ya kuomba na mambo ya kumwomba Mungu. Mara nyingi baadaye, Yesu aliwafundisha wanafunzi wake zaidi juu ya maombi. Wakati mwingine aliwafundisha kwa kuwasimulia hadithi. Labda twaweza kujifunza mengi zaidi juu ya maombi kwa kusoma hadithi hizi.

Majira fulani ya mwaka katika nchi ya Uyahudi (Palestina) kuna joto jingi sana wakati wa mchana. Kwa sababu hii, wasafiri wengi husafiri wakati wa usiku. Usiku ni

baridi na huwapa wasafiri muda mzuri sana kusafiri. Mara nyingi nyakati za Zamani wasafiri walimaliza safari zao usiku wa manane.

Siku moja, msafiri mmoja alikwenda kwa nyumba ya rafikiye usiku wa manane. Alikuwa amechoka, na alitaka kupumzika huko kabla ya kuendelea na safari. Na tena alikuwa na njaa na alihitaji kula. Lakini ilikuwa bahati mbaya. Hakuna mtu aliyejua kwamba yujaja,



na rafiki hakuwa na chakula cho chote cha kumpa.

Kaika nchi hii mikate iliokwa kila asubuhi na kuliwa. Usiku hapakuwa na mkate wo wote uliobakizwa. Msafiri huyu hakuweza kupata mkate wa kula. Rafikiye aliudhika sana kwa sababu hakuweza kumpatia cho chote kula. Lakini alikuwa na wazo la kufanya!

Alikimbia akaenda kwa nyumba ya jirani yake. Akamwambia, "Rafiki, mgeni amekuja, lakini hatuna chakula cha kumpa ale. Tafadhali, nikopeshe mikate mitatu."

Jirani huyo alikasirika sana. Ilikuwa ni usiku wa manane na kila mtu nyumbani mwake alikuwa amelala. Hata milango ilikuwa imelungwa ili kuwazuia wevi. Basi alimwambia, "Usinitaabishe. Tumelala kitandani mimi na watoto wangu. Siwezi kuondoka nikupe mikate. Hii ni kazi nyingi."

Rafiki huyu alikataa kuondoka. Aliendelea kummwomba jirani yake mikate. Alikataa kupoka jibu la jirani yake la kusema "Ia." Alikuwa na hitaji, kwa hivyo alitaka msada. Baadaye kidogo, yule jirani aliondoka na kumpa mikate. Alijua kwamba hataweza kulala mpaka atakapomsaidia yule mtu.

Yesu alisimulia hadithi hii kuwaonyesha wanafunzi wake ukweli. Ikiwa jirani yule mwenye choyo aliweza kumpa rafiki yake mikate alipoendelea kummwomba, ni kweli kwamba Yesu aweza kufanya mengi zaidi ya hayo. Tukionmba bila kuchoka

kwa kutaka vitu tunayo hitaji, Mungu atajibu hilo ombi letu. Pengine itachukua muda mrefu. Lakini tuombe mara kwa mara kwa ajili ya kitu tunachohitaji.

Baadaya Yesu kumaliza kusimulia hadithi hii aliwauliza wanafunzi wake maswali mengine ya ajabu. Alisema, "Ukimwomba baba yako mkate, je, atakupa jwe?" La! Ukimwomba baba yako samaki, atakupa nyoka. "Je, mtoto akimwomba babaye yai atampa nge?"

Wanafunzi wa Yesu walijua kwamba hawawezi kuwatendea watoto wao mambo kama haya. Na ikiwa walijua kuwapa watoto wao vitu vizuri, ni kweli kwamba Mungu atawapa wafuasi wake vitu vizuri mno kuliko hivyo yao. Mungu atajibu maombi yetu na kutupa vitu tunavyohitaji hasa.

KAZI YA KUFANYA:

Yesu alitupa mfano wa sala tunaaita "Sala ya Bwana." Soma sala hii, (Mathayo 6:9-13) hatafu andika namba moja hadi saba katika nafasi zilizoachwa kuonyesha vile sentesi hizi zinafaa kufuatana.

_____ Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasameheyo wadani wetu.

_____ Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.

_____ Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.

_____ Ufalme wako ujc.

_____ Utupe leo riziki yetu.

_____ Baba yetu ulie mbinguni, jina lako litukuzwe.

_____ Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele, Amina.

Baba walezi (baba wa hapa ulimwenguni) wa watoto hawapi watoto wao vitu ambayo vitawadhuru. Chora mstari kutoka kwa kila swali hadi kwa jibu lililo sawa.



Ni nini ambacho baba hatampa mtoto wake anaye-mwomba mkate?



Ni nini ambacho baba hatampa mtoto wake anaye-mwomba samaki?



Ni nini ambacho baba hatampa mtoto wake anaye-mwomba yai?



Baba yetu aliy mbinguni atawapa nyinyi vitu vingi zaidi yecma ikiwa minamwuliza au minamwomba yeye.

Yesu aliwambia wanafunzi wake hadithi juu ya msafiri mmoja. Andika jibu lililo sawa katika nafasi hiyo iliyo hapa chini.

Usiku moja wa manane, mtu mmoja alibisha mlangooni mwa jirani yake. Alitaka kukopa _____

kwa sababu _____

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Ombeni, nanyi mlapewa; tafuteni nanyi mlaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa." Luka 11:9

Mara nyingi twaomba mara moja tu kwa kutaka kitu fulani. Na Mungu asipojibu ombi hilo letu, tunaacha kuomba tena. Hata Yesu anapojua hitaji letu tusikome, bali tundelee tu kuomba. Yatupasa kuomba mara nyingi kwa ajili ya kitu tunachohitaji kwa sababu Mungu hujajibu maombi yetu. Wakati mwingine Mungu aweza kujibu ombi letu kwakusema, "Ia." Wakati mwingine aweza kusema, "Ngonica." Lakini kifungu chetu cha kukumbuka kinatuambia ya kwamba Mungu atatujibu kila siku tunapomwomba.


VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA

KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved



Sura ya Kumi na Moja

YESU AELEZA JINSI YA KUMWEKA KWANZA MAISHANI

MASOMO YA BIBLIA: Luka 18:18-30

Watu wengi waliomjia Yesu walikuwa na maswali ambayo walitaka ayajibu. Hata siku moja, mtawala mmoja akaja. Alipiga matogi mbele ya Bwana, akanza kusema.

Mtawala: Mwalimu mwema, nifanye nini ili nipate kuurithi uzima wa milele?

Yesu: Mbona unaniita "Mwema?" Hakuna aliye mwema ila mmoja, naye ndiye Mungu. Wazijua amri; usizini, usiue, usibe, usishuhudie uongo, waheshimu baba yako na mama yako.

Mtawala: Hayo yote nimeyashika tangu utoto wangu.

Yesu: Umepungukiwa na neno moja bado. viuze uliyo navyo vyote, ukawagawanyie maskini. Nawe utakuwa na hazina mbinguni. Na unapofanya hivi, njoo unifuata.

Yule mtawala aliposikia hivyo alihuzunika sana. Alikuwa tajiri mwenye mali nyingi. Yesu alijua kwamba mtawala huyu tajiri alihuzunika. Alijua kwamba hakutaka kuuza mali yake. Yesu akamwambia:



Yesu: Ni vigumu sana kwa mtu tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. Ni yepesi ngamia kupitia katika tundu la sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu.

Kulikuwa na umati wa watu karibu nao. Waliposikia maneno hayo ambayo Yesu aliyasema, hawakuelewa. Mtu mmoja kati yao akamwuliza Yesu swali.

Mtu huyo: Ni nani basi awezaye kuokoka?

Yesu: Yasiyowezekana kwa mwanadamu yawezekana kwa Mungu.

(Petro, mmoja wa wanafunzi wake akaanza kusema.)

Petro: Sisi tumeviacha vitu vyetu vyote na kukufuata.

Yesu: Ndiyo, mmeviacha, lakini nawaambia, hakuna mtu aliyearcha nyumba, au mke, au ndugu, au wazazi, au wana, kwa ajili ya ufalme wa Mungu, asiypokea zaidi mara nyingi katika zamani hizi, na katika ulimwengu ujao uzima wa milele.

Mtawala huyu tajiri alikuwa akitaka jibu la swali lake. Alikuwa ameishi kulingana na amri na alimpenda Mungu. Lakini alivipenda vitu vingine zaidi kuliko Mungu.

Yesu alipomwambia auze mali yake, mtawala huyu tajiri alihuzunika sana. Alimpenda Mungu, lakini alipenda fedha zake zaidi kuliko Mungu. Alihamani sana utajiri na akaufanya kitu cha kwanza maishani mwake.

Yesu naye alihuzunika. Alihuzunika kwa sababu mtawala huyu tajiri hakumpenda kuliko vyote alivyokuwa navyo. Mtawala huyu aliondoka, akaenda zake nyumbani. Hakuwa na nia ya kumweka Kristo kwanza maishani mwake.


Mara nyingi ni vigumu sana kwa tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. Hupenda fedha zake mno na kuchagua kuishi katika oja zake na kukataa kujitoa kwa Mungu. Yesu alijua jambo hilo. Lakini alijua pia kwamba Mungu ndiye aliyefanya uwezekano wa mambo yote. Yasiyowezekana kwa mwanadamu kwa Mungu yawezekana. Yesu aweza kugeuza moyo wa tajiri na kumfanya ampende Mungu kuliko fedha zake.

Wengi wetu si matajiri, lakini twaweza kuwa na vitu vingine badala ya fedha maishani mwetu. Je, nikitu kipi ambacho ni cha muhimu sana maishani mwako? Pengine tunapomweka Yesu kwanza maishani mwetu inatubidi kuacha vitu fulani kwa sababu havilingani na mapenzi ya Mungu maishani mwetu. Yesu alimwambia Petro ya kwamba chochote tunachokiacha kwa ajili ya Mungu si cha muhimu. Tutapokea baraka nyingi zaidi kwa sababu tulimweka Mungu kwanza maishani mwetu. Hatutapata tu furaha halisi hapa ulimwenguni tu bali hata mbinguni pia.

Je, ina maana gani kwako kumweka Kristo kwanza maishani mwako?

KAZI YA KUFANYA

Katika picha iliyo hapo chini mtawala tajiri anamwuliza Yesu swali. Andika swali hilo ambalo mtu huyu alimwuliza Yesu.



Yesu alimwambia mtawala huyu tajiri atanye mambo fulani kisha atakuwa na hazina mbinguni. Andika namba (1,2,3) ya mambo hayo ambayo Yesu alimwambia.

___ Njoo unifuata.

___ Viuzeulivyo navyo vyote.

___ Ukawagawanyie maskini.

Chora duara kwa majina yaliyo hapo chini ya watu ambao Yesu alisema kwamba wana shida ya kuingia ufalme wa Mungu.

Wazee Maskini Wema Wenye mali Vijana Wenye huzuni

Piga mstari chini ya jibu lililo sawa.

Yesu alisema kwamba ni vigumu kwa tajiri kuingia ufalme wa Mungu kuliko:

Chombo (merikebu) kuabiri katika nchi kavu.

Ngamia kupita katika tundu la sindano.

Weka alama ya (X) kwenye mstari ulio kandoya sentensi inayoonyesha zawadi ambayo Yesu aliwaahidi wale

ambao wanaacha nyumba zao na jamaa zao ili kumtumikia.

___ Mali nyingi na heshima hapa ulimwenguni.

___ Baraka nyingi hapa ulimwenguni.

___ Uzima wa milele mbinguni.


KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Basi, kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu." Luka 14:33

Kuna watu wengi ambao ni kama mtawala yule tajiri. Hawana nia ya kumpa Kristo nafasi ya kwanza maishani mwao. Wengine wanaweka fedha katikanafasi yakwanza maishani mwao. Labda wengine wanaruhusu kitu kingine kiwe cha kwanza maishani mwao. Ikiwa twampa Yesu nafasi ya kwanza maishani mwetu kama vile anavyo tuambia basi tunapokea kitu ambacho ni kizuri zaidi kuliko fedha au anasa. Tunakuwa na baraka hapa ulimwenguni, na baraka mbinguni.

mwenye dhambi aliyepotea. Alimtaka Yeau kumwondolea udanganyifu wake na uongo.

Zakayo alijua kwamba Yesu alikuwaamejaa upendo. Yesu alikubali kumsamehe na kumfanya kuwa mwaminifu. Zakayo alifurahi sana kwa sababu Yesu alikubali kumsamehe dhambi zake! Katika picha hiyo ya moyo iliyoko upande wa kulia, andika mambo ambayo unafikiri yalikuwa ndani ya moyo wa Zakayo baada ya Bwana kumsamehe dhambi zake.



VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA

KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

© Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved

Sura ya Kumi na Mbili

YESU AMWOKOA MTU ALIYEKUWA MTINI

MASOMO YA BIBLIA: Luka 19:1-10

Zakayo. Hili ni jina la ajabu kwa mtu kuwa nalo. Maana yake ni "msafi" au "mwenye haki" Lakini mtu mmoja ambaye Yesu alikutana naye, ambaye jina lake ilitwa Zakayo akustahili jina hili zuri.

Zakayo alikuwa mtoza ushuru. Alikuwa Myahudi lakini alitumikia serikari ya Kirumi. Wayahudi walikuwa maadudi wa Warumi na waliwachukia sana. Pia walimchukia Zakayo kwa sababu alitumikia serikali ya Kirumi. Kila wakati alipokusanya ushuru, Zakayo alichukua fedha zaidi asiyostahili. alitajirika sana kwa kutumia mpango huu wa hila.

Zakayo alikaa katika mji wa Yeriko, maili 15 hivi kutoka Yerusalemu. Afisi ya watoza ushuru ilikuwa hapa Yeriko, na Zakayo alikuwa mkubwa wa watoza ushuru.

Alikuwa na kazi kubwa, lakini yeye alikuwa mtu mfupi wa kimo.

Hata siku moja, Zakayo alisikia kwamba Yesu alikuwa anakuja Yeriko. Alikuwa amekwisha kusikia mambo mengi juu ya Yesu hata akawa na tamaa ya kumwona. Labda alifikiri kwamba Yesu atampa kitu ambacho fedha zake hazivezikununua. Aliposogea karibu na umati ule wa watu waliomfuata Yesu, hakuweza kumwona. Alikuwa mfupi wakimo na ilikuwa vigumu



kwake kumwona Yesu kati ya umati huo wa watu.

Angewezaje basi kumwona Yesu? Zakayo hakufa moyo. alitangulia mbio mbele ya umati, akapanda juu ya mti. alikaa hapo mtini mpaka Yesu alipoptia njia hiyo. Na sasa aliweza kumwona Yesu barabarani!

Yesu alipokuwa akipitia karibu na mti ule, alitazama juu, akamwona Zakayo. "Zakayo," Yesu akmwambia, "Shuka upesi. Leo imenipasa kushinda nyumbani mwako."

Zakayo alishangaa mno. Yesu aliwazaje kulijua jina lake? Ni kwa ajili gani Yesu alitaka kukaa nyumbani mwa Zakayo? Zakayo alishuka haraka. Akamkaribisha Yesu kwa furaha nyumbani mwake. Na zaidi ya hayo, zakayo pia alimpokea Yesu moyoni mwake. Aligeuka na kuwa mwana wa Mungu. Siku hiyo yote Yesu alishinda nyumbani mwa Zakayo.

Watu wa Yeriko walianza kunung'unika. Walulizana wao kwa wao wakisema, "Kwa nini Yesu yuala pamoja na mtu mwenye dhambi kama huyu?" Mmoja wao akasema, "Zakayo ni mkubwa wa watu wenye dhambi." Watu hawa walikuwa wamesahau kwamba wao pia walikuwa wenye dhambi. Yesu alikuwa amekuja kutafuta na kuwaokoa watu wote wenye dhambi, hata Zakayo. Lakini jirani zake Zakayo hawakujua mabadiliko yaliyokuwa moyoni mwake.

Yesu alipokuwa akijitayarisha kuondoka, Zakayo alikuwa na jambo moja muhimu sana la kusema. Alisimama akasema, "Bwana, nusu ya mali yangu nawapa mskini. Na ikiwa nimenyang'anya mtu kitu kwa hila namrudisha mara nne." Mvujiza ulikuwa umefanyika maishani mwa Zakayo. Jamaa, rafiki zake, na hata maadui zake hawakuweza kuamini yale waliyoyasikia.

Zakayo alikuwa amemweka Kristo kwanza maishani mwake. Na sasa alitaka kuepukana na hila zake. Mtoza ushuru huyu mwenye choyo, na ambaye alichukwa, alikuwa akiitubu sasa hadharani kwamba alikuwa amewadanganya wengine. Alitaka kuwaonyesha watu mabadiliko yaliyomfikia moyoni mwake. Na kwa vile sasa alimwamini Yesu, alitaka kuwafanyia watu mambo mema.

Yesu alipendeza sana na Zakayo. Kwa sababu ya mabadiliko maishani mwa Zakayo, "Leo wokovu umefika nyumbani humu." Yesu alipokuwa akiondoka, aliwambia watu wote habari kuhusu kusudi lake la kuja ulimwenguni. Alisema, "Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea."

Vile Yesu aliyomtafuta Zakayo na kumwokoza, ndiyo anavyowatafuta na kutaka kuwaokoa wenye dhambi wote. Tukimweka kwanza maishani mwetu, maisha yetu yatabadilika kuwa kama maisha ya Zakayo.

KAZI YA KUFANYA

Kata neno lisilo swa katika sentensi zifuatazo, kisha andika neno lililo sawa katika msitari ulio kando ya kila sentensi.

____ Zakayo, mkubwa wa watoza ushuru, alikuwa maskini.

____ Yonathani alitaka kumwona Yesu, lakini hakuweza kwa sababu ya umati wa watu.

____ Zakayo alikuwa mtu mrefu.

____ Alikimbilia mbele ya umati akapanda juu ya mwamba.

Maisha ya Zakayo yaligeuka kuwamema wakati ule alipokutana na Yesu. Twaajuaje ya kwamba jambo hili ni kweli? Andika neno "Ndiyo" kando ya sentensi ambayo ni kweli.

____ Zakayo alisema kwamba alibadilika.

____ Zakayo alirudisha mara nne mali aliyowanyang'anya maskini kwa hila.

Yesu alisema kwamba alikuwa amekuja kufanya kazi maalum. Andika alama hii (X) kando ya sentensi zenye sababu zilizomfanya Yesu kuja ulimwenguni.

____ Kutafuta na kuokoa watu wanaofikiri kwamba ni wema.

____ Kutafuta na kuwaokoa watu waliopotea dhambiini.

____ Kuwafanya wenye dhambi kuburidikia moyoni mwao.

____ Kama ungali kuwa katika umati ule siku ile ya furaha ungalinwona

Zakayo pamoja na Yesu. Andika herufi "M" kando ya sentensi zenye makosa, na uandike herufi "K" kando ya sentensi ambazo ni kweli.

____ Zakayo alitangulia mbio mbele ya umati wa watu akapanda mti ili aweze kumwona Yesu.

____ Zakayo alikuwa mtoza ushuru mwenye uongo ambaye alichukwa.

____ Mti ambaye Zakayo alipanda juu ulikuwa mtende.

____ Yesu alimwambia Zakayo ya kwamba alitaka kuwa mgeni wake.

Yesu aligeuza maisha ya Zakayo hata akawapa mara nne maskini mali aliyowanyang'anya kwa hila.

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA:

"Uniondolee ubatili na uongo."

Mithali 30:8

Wakati Zakayo alipomwona Yesu, alitambuahali yake mwenyewe. Alipomwanguka Mwokozi, aliona jinsi moyo wake ulivyojaa dhambi. Bila shaka moyo wake ulionekana kama picha hiyo iliyoko upande wa kushoto. Alijua kwamba alikuwa


VIJANA TUJIFUNZE BIBLIA

MWAKA WA KWANZA KITABU CHA KWANZA

KUJIFUNZA HABARI ZA YESU

J1-1Ps

©Copyright 1987, Baptist Publications House, All Rights Reserved



Sura ya Kumi na Tatu

SOMO LA MARUDIO

Wiki hii tutarudia masomo yote ya miezi mitatu iliyopita. Fanya kazi yote inayofuata. Ikiwa huwezi kukumbuka majibu angalia andiko linalotolewa. Na katika andiko hilo utaweza kupatamajibu yaliyo sawa.

"Yesu alikuja



katika Ziwa la Galilaya ambako nikuwa mvuvi. Aliniambia nitweke mpaka kilindini, nikashushe nyavu zangu. Nilipofanya hviyo, nilishika

samaki wengi mno hata nyavu zangu zikaanza kukatika. Niliporudi tena ukingoni Yesu alikuwa pale na akasema ya kwamba atanifanya mvuvi wa _____"

SIMONI PETRO (Luka 5:1-11)

Soma Luka 5:10 na uwataje watu wengine wawili ambao walikuwa pamoja na Simoni, _____ na _____ Watu hawa waliacha vyombo vyao na _____ wakamfuata Yesu. (Luka 5:11)



Mimi pamoja na wenzangu wengine tisa tulimjia Yesu. Sisi sote tulikuwa wenye ukoma. Yesu alituhurumia siku hiyo. Alituingia

_____ Tulipofanya hivyo tulitakasika." Ni wangapi kati ya wagonjwa hawa walimshukuru

Yesu? _____ Je, alikuwa ametoka
(wa kabila gani) wapi.

Wakati mmoja, Bwana aliwachagua watu _____ kumtanguilia kwenda katika vijiji na miji. Aliwatuma _____ na _____. Yesu aliwaambia kwamba _____ yalikuwa mengi, lakini watenda kazi walikuwa _____. Iliwapaswa _____ ili Bwana wa mavuno apeleke watenda kazi wengi. Watu hawa waliambiwa _____ kitu cho chote. Basi, waliondoka wakaenda katika miji na vijiji hivi. Na waliporudi, walisema, "Bwana, hata _____ wanatuii kwa jina lako."

"Hadithi yangi" inaanza katika Luka 15, kifungu cha 11 na 12. Soma vifungu hivi kwanza, Je, waikumbuka hadithi yangu na yale yaliyonipata?



"Nilichukua fedha ambazo b a b a aliniwekea, n i k a e n d a zangu nchi ya mbali. Na huko nilitumia fedha zangu zote, nikabaki bila cho chote, wala chakula. Nilikata shauri kurejea _____ (kifungu cha 18). Baba yangu alifurahai mno kuniona, hata akaanpa joho, na _____ ya kutia kidoleni, na _____ ya kuvaa kwa miguu. Nilikuwa nimepotea, na sasa nimeonekana."

Soma Luka 18:22-23, na ujibu maswali juu ya mtu huyu.



"M i m i ndiye _____ aliyekuja kwa Yesu. Nili-kuwa na swali muhimu la kumwuliza. Nilitaka kujua k a m a i l i n i p a s a kufanya _____"

Yesu aliniambia niuze _____ na niwagawanyie _____ Niliposikia haya, nilihuzunika sana kwa sababu; nilikuwa tajiri sana."

"Bila shaka unanikumbuka! Nina hadithi nzuri ya kusimulia. Kama utasoma Luka 19:1-10, utapata kuona ya kwamba mimi ni mtu gani, na utaweza kujibu maswali haya."



"Jina langu ni _____, na nilikaa katika mji wa _____. Yesu alipokuja katika mji wetu, ilinibidi _____ juu ya _____ ili niweze kumwona. Alikuja karibu nami akaanila kwa jina langu, kisha akasema kwamba imempasa kushinda _____"

Yesu alibadilisha maisha yangu nikawa mwamini, nikakata kuhakikisha upendo wangu. Nilikuwa tayari kutoa _____ ya mali yangu kwa maskini, na kwa wale niliowanyang'anya kwa hila nawarudishia mara _____ zaidi. Siku ile, wokovu ulifika kwangu na kwa _____ yangu. Yesu alisema kwamba alikuwa amekuja _____ na _____ kile kilichopotea."